**102/1**

**KISWAHILI – INSHA**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**102/1**

**Insha**

1. – Mtindo wa mahojiano uzingatiwe
   - Maswali yaelekezwe upande mmoja yaani, kutoka kwa mwandishi habari kwelekea kwa mwanasiasa.
   - Jinsi ya kuendeleza kaunti
     - ✓ Ujenzi barabara
     - ✓ Ujenzi wa shule
     - ✓ Usambazaji maji
     - ✓ Usambazaji stima (umeme)
     - ✓ Mikopo kwa wananchi kwa riba ya chini.
     - ✓ Kuwajibika katika matumizi ya pesa za eneo bunge.
     - ✓ Kuimarisha usalama ili kuvutia wawekezaji

2. – Hii ni insha ya mjadala
   - Kimsingi insha hii ina sehemu mbili; mtoto wa kike na jinsi anainuliwa huku pia kukiwa na mtoto wa kiume na jinsi amedhalilishwa.
   - Mtahiniwa aweza kuwa na hoja nyingi upande mmoja mradi kila upande uwe na angalau hoja tatu.
   - Mwisho yafaa mtahiniwa atoe msimamo wake kuhusu mjadala huu. Je yeye aunga upande gani?
     Baadhi ya hoja za kuunga mkono kuinuliwa kwa mtoto wa kike.
   - Amedhalilishwa kwa miaka na mikaka.
   - Amedhalilishwa na utamaduni.
   - Anapigwa na waume na pia mabwana zao.
   - Anofanyishwa kazi nyingi za nyumbani hususa za jikoni.
   - Anaozwa mapema tena kwa wazee.
   - Anajisiwa, anabakwa, achafuliwa.
   - Anyimwa nafasi ya kupata elimu.
   - Anyimwa urithi wa wazaziwe na mumewe
   - Apashwa tohara ya lazima

- Arithiwa na shemejize mumewe aagapo.
- Apatapo mimba afukuzwa shuleni.

**Jinsi mtoto wa kiume amedhalilishwa**

- Miradi mingi na hela nyingi zimetengewa mtoto wa kike.
- Mashirika mengi yamebuniwa kutetea mtoto wa kike na wanawake, mfano chama cha maendeleo ya wanawake.
- Alama za wasichana kuingia vyuo vikuu zimeshushwa kiasi.
- Shule za mabweni za wasichana nyingi ilhali mtoto wa kiume ameaachwa kumezwa na magenge kama vile munguki na pombe haramu.
- Wakati jamii inamtetea mtoto wa kike ilhali mtoto wa kiume ameachwa ajiamulie hatima yake bila mtetezi wa moja kwa moja.

3. – Hii ni methali
   - Maana ya methali izingatiwe
     Mtahiniwa atunge kisa/ visa kitakachodhihirisha kuwa yeyote ajiingizaye kwenye matatizo / majango basi haumii yeye tu bali pia wanaomhusu.
   - Methali ina pande mbili “mchuma janga” na “hula na wakwao”.

4. Mwanafunzi amalizie kwa maneno aliyopewa
   - Mwanafunzi asipofanya hivyo atakuwa amepotoka
   - Kisa kikuzwe kikamilifu
   - Zingatia ufaafu wa kisa cha mwanafunzi.